
JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BARAZA LA TAIFA LA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI




# JARIDA LA BARAZA LA TAIFA LA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI (NEEC) - 2023

# NENO KUTOKA KWA KATIBU MTENDAJI



**BENG'I M. ISSA**
Katibu Mtendaji wa Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi

www.uwezeshaji.go.tz

KARIBU katika toleo la nane la Jarida la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ambalo limekusanya taarifa muhimu za mafanikio ya Kiuwezeshaji kutoka Serikalini, wadau wa maendeleo na Sekta binafsi ambazo zimepelekea kuibuliwa kwa fursa mpya za kiuchumi katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2022/2023 nchini Tanzania.

Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC) linatambua na kuthamini jitihada zinazochukuliwa na Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt Samia Suluhu Hassan ambaye amekuwa mstari wa mbele kuhakikisha Watanzania wananufaika na keki ya Taifa katika mazingira ya usawa na uwazi bila kujali dini, jinsia na itikadi ya vyama vya kisiasa.

Baraza la Uwezeshaji pia linathamini juhudi zinazofanywa na sekta zote za kiuchumi kuanzia ngazi za Halmashauri, Mikoa mpaka Taifa katika kutekeleza Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ya Mwaka 2004 ambayo inasimamiwa na kuratibiwa na Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi.

Ndugu Msomaji, Jarida hili litakuangazia kwa mapana jitihada zilizofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita katika kukuza pato la mtu mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla kupitia fursa mbalimbali kama vile zabuni, mafunzo, malighafi na ajira kwenye miradi ya kimkakati, uendelezaji wa Biashara, Mifuko ya Uwezeshaji, Program za Uwezeshaji na Vituo vya Uwezeshaji.

Miongoni mwa mambo makubwa yaliyofanyika katika mwaka huu wa fedha ni pamoja na Maonyesho ya Mifuko na Program za Uwezeshaji ambayo mwaka huu yalifanyika katika viwanja vya Mwanga, Mkoa wa Kigoma ikiwa ni maonyesho ya sita ya Mifuko ya Uwezeshaji Kiuchumi huku lengo likiwa ni kusogeza karibu zaidi huduma za Uwezeshaji kiuchumi kwa Wananchi kupitia mifuko hiyo.

Ndugu msomaji, Jarida hili linakupa nafasi ya kufahamu utendaji wa Mifuko hiyo na miradi mbalimbali ya Kimkakati ambayo inaweza kukusaidia kutambua fursa za Kiuwezeshaji ambazo zinaweza kukusaidia kuongeza pato lako.
Mifuko ya Uwezeshaji imekuwa rafiki zaidi kwa wananchi ambapo huwagusa watu wa matabaka yote mpaka wale wanaokosa sifa za kukopesheka kwenye Taasisi za Kifedha ikiwemo Mabenki.

Mpaka kufika Aprili, 30, 2023 Serikali imefanikiwa kuanzisha jumla ya Mifuko ya Uwezeshaji Kiuchumi 62 huku ikiweka mazingira rafiki kwa Sekta Binafsi kuweza kuanzisha mifuko kumi (10) ambapo kwa ujumla wake imefanikiwa kutoa jumla ya mikopo yenye thamani ya Shilingi Tilioni 6.1 na wanufaika wakubwa zaidi ni wanawake ambao wanafikia asilimia 54.

Serikali pia imepanua huduma za Uwezeshaji kupitia vituo vya Uwezeshaji ambavyo uanzishwaji wake umekua kwa kasi kutoka kituo kimoja kilichoanzishwa Novemba 18, 2018 katika Manispaa ya Kahama mpaka vituo 19 mwaka 2023.

Hata hivyo jitihada zinaendelea kufanyika huku lengo likiwa kila Halmashauri kuwa na kituo kimoja cha Uwezeshaji ambacho kitakusanya huduma zote muhimu kuanzia utoaji wa mikopo, urasimishaji wa biashara, huduma za masoko na elimu ya ujasiriamali.

Ndugu msomaji, katika jarida hili pia zipo simulizi mbalimbali za watu waliofanikiwa kwenye nyanja za kiuchumi ambapo jitihada na mbinu walizotumia zinaweza kutoa mafunzo ambayo yanaweza kukuwezesha kupata maarifa na taarifa ya kusonga mbele.

Baraza linakutakia usomaji mwema wa Jarida hili ambalo litakuletea mwanga na kuchukua hatua ya kuziendea fursa za Uwezeshaji zilizopo katika maeneo mbalimbali ikiwemo Serikalini na Sekta binafsi.




# TRILIONI 6.1 ZATOLEWA KWA WAJASIRIAMALI

KIASI cha Shilingi Trilioni 6.1 zimetolewa kama mkopo na ruzuku kwa wajasirimali milioni 8.6 kupitia Mifuko na Program mbalimbali za Uwezeshaji kutoka Serikalini na Sekta binafsi.

Katibu Mtendaji wa Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC), Beng'i Issa ameeleza hayo wakati wa maonyesho ya Mifuko na Program za Uwezeshaji yaliyofanyika kwenye Viwanja vya Mwanga Centre huko Kigoma Mjini kuanzia tarehe 21 hadi 27 Mei, 2023.

Beng'i amesema kuwa hadi kufikia mwezi Machi mwaka huu, Mifuko na Programu hizo za uwezeshaji zimewezesha kutolewa kwa mikopo hiyo kwa wajasiriamali hao ambao kati yao wajasiriamali wanawake wakiwa ni milioni 4.7 na wanaume milioni 3.9, ambapo ajira milioni 17.6 zimetengenezwa.

Katibu huyo Mtendaji wa Baraza alisema kuwa serikali imejipambanua katika kutekeleza Mpango wa uwezeshaji wananchi kiuchumi, hivyo uwepo wa mifuko hiyo ni utekelezaji wa mpango huo na kwamba maonesho yaliyofanyika Kigoma ni sehemu ya utekelezaji wa azma ya Serikali ya Awamu wa Sita kuufanya Mkoa huo kuwa wa kimkakati kiuchumi.

Wakati huo huo, Meneja wa Mawasiliano wa Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), Christina Njovu nae alisema kuwa ni jambo muhimu kwa wajasiliamali kusajili majina ya biashara zao na kampuni ili ziweze kutambulika ndani na nje ya nchi kwa urahisi.

Njovu alisema kuwa BRELA inasajili leseni kundi A ambazo kiasi kikubwa zinahusu wafanyabiashara wanaofanya biashara za kuvuka mpaka hivyo wajasiriamali na wafanyabiashara wa Mkoa Kigoma ambao wako mpakani imewapa nafasi nzuri ya kufanya biashara ya kuvuka mpaka na nchi jirani za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) na Burundi.

Meneja huyo wa BRELA alisema kuwa katika upatikanaji wa mikopo kwa wafanyabiashara na wajasiriamali wanaovuka mpaka kusajili kampuni na majina ya biashara ni mambo muhimu na kwa sasa usajili huo unafanyika kupitia njia ya mtandao na wajasiriamali wanaweza kujisali mahali popote walipo.

Wakati wa ufunguzi wa Maonyesho hayo, Mkuu wa Mkoa wa Kigoma, Kamishna Mstaafu wa Jeshi la Zima Moto, Thobias Andengenye, alisema kuwa maonesho ya Sita ya mifuko na programu za uwezeshaji wananchi kiuchumi ni chachu kwa watu Kigoma katika kupata habari na taarifa ambazo zinasaidia kuimarisha shughuli zao za uzalishaji na uwekezaji.



# SERIKALI YASISITIZA MAMBO MAZURI KWA WAJASIRIAMALI

WAZIRI Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mh. Kassim Majaliwa Majaliwa (MB), amesema kuwa Serikali itaendelea kuweka mazingira mazuri kwa wajasiriamali ya kuwezesha kupata mikopo na maeneo ya biashara, ili shughuli zao ziwe na tija katika kukuza uchumi.

Amesema hayo akifunga maonesho ya Sita ya Mifuko na Programu za uwezeshaji wananchi kiuchumi yaliyofanyika Mjini Kigoma katika hotuba iliyotolewa kwa niaba yake na Mkuu wa Mkoa Kigoma, Kamishna Mstaafu wa Jeshi la Zima Moto na Uokoaji Mh.Thobias Andengenye.

Alibainisha kuwa shughuli za wajasiriamali zina mchango mkubwa katika kukuza kipato chao kupitia vikundi vyao, mtu mmoja mmoja katika kukuza ajira sambamba na kukuza uchumi wa nchi.



Alisema kuwa kupitia mifuko 72 inayotoa ruzuku, mikopo na huduma mbalimbali, Serikali itaendelea kuwawekea mazingira mazuri na wezeshi wajasiriamali ikiwemo kuwaunganisha na mifuko na taasisi zinazotoa mikopo, elimu, ithibati ya bidhaa, urasimishaji wa bidhaa, elimu ya kuandaa wazo na mpango wa biashara.

Awali Katibu Mtendaji wa Baraza la Taifa la Uwezeshaji wananchi kiuchumi (NEEC), Bibi Beng'i Issa, alisema kuwa maonesho ya Mifuko na Program za uwezeshaji wananchi kiuchumi zimekuwa na tija kubwa kwa kusogeza huduma kwa wananchi.

Naye Ofisa Usajili wa Biashara na Leseni kutoka (BRELA), Stanislaus Kigosi alisema kuwa kumekuwa na changamoto katika taratibu za usajili wanazopata watu mbalimbali, hivyo ushiriki wao kwenye maonesho mbalimbali yanasaidia kupata watu wengi ambao wanafika kwenye banda lao na kutatua changamoto hiyo.

Alisema kuwa pia wamekuwa wakitumia maonesho kupita kwenye mabanda ambayo yana washiriki kutoka mikoa mbalimbali, ambapo wanakutana nao na kuwaelewesha umuhimu wa kusajili majina ya biashara zao na taratibu nyingine ili kuwawezesha kukidhi vigezo vya biashara za kuvuka






# PASS TRUST YABEBA TUZO YA UWEZESHAJI

MFUKO wa Pass Trust umefanikiwa kuondoka na tuzo ya nafasi ya kwanza katika maonyesho ya Mifuko na Program za Uwezeshaji yaliyofanyika katika Mkoa wa Kigoma.

Mkurugenzi Mtendaji wa PASS Trust, Yohane Kaduma alipokea tuzo hiyo kutoka kwa Mgeni rasmi, Mkuu wa Mkoa wa Kigoma Kamishna Mstaafu wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Mhe. Thobias Andengenye baada ya mshindi wa nafasi ya kwanza Kitaifa katika kundi la Mifuko na Programu za Uwezeshaji nchini Tanzania.

Tuzo hizo zimetolewa kwenye Hafla ya kuitimisha Maonesho ya 6 ya Mifuko na Programu za Uwezeshaji 2023 yaliyofanywa na Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC) katika Uwanja wa Mwanga, Mkoa wa Kigoma ambayo yaliendana kauli mbiu ya "Uwezeshaji Kiuchumi kupitia Mabadiliko ya Kidigital".

Mfuko wa Self Microfinance ulifanikiwa kushika nafasi ya pili na nafasi ya tatu ilienda kwenye mfuko wa UCSAF.
Upande wa tuzo zilizoenda kwenye Mikoa nafasi ya kwanza ilishirikiriwa na Mkoa wa Kigoma huku nafasi ya pili ikikamatwa na Mkoa wa Shinyanga.

Akizungumza kuhusiana na tuzo hizo, Katibu Mtendaji wa Baraza la Uwezeshaji Bibi Bengi Issa amesema kwamba utaratibu wa tuzo hizo unalenga kuthamini na kutambua jitihada zinazofanywa na Mifuko ya Uwezeshaji katika kusaidia wajasiriamali, wakulima na wafanyabiashara.

"Hili ni zoezi huru ambalo hufanywa na jopo maalum la wataalam kwa kuzingatia vigezo vilivyowekwa na tumekuwa tukifanya hivi kila mwaka kama sehemu ya kutambua na kuthamini jitihada zinazofanywa na Mifuko ya Uwezeshaji"alisema Bibi Bengi Issa.

# WAJASIRIAMALI WATENGEWA MAZINGIRA WEZESHI YA MASOKO



SERIKALI ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya Mh. Rais DK.Samia Suluhu Hassan imezidi kutengeneza mazingira wezeshi kwa wajasiriamali kupata masoko ndani na nje ya Nchi.

Hayo yamethibitishwa na Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe katika hafla ya utoaji tuzo za Wanawake wanaozalisha bidhaa za Viwandani zilizoandaliwa na Chama cha Wafanyabiashara Wanawake Tanzania (TWCC) iliyofanyika katika ukumbi wa Mlimani city Jijini Dar es Salaam.

Alisema kuwa Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine wakiwemo, TWCC imekuwa ikitambua bidhaa zinazo zalishwa na kwamba kwa kupitia majukwaa yao kumekuwa na fursa nyingi zinazolenga kuwasaidia kufikisha bidhaa zao kwenye masoko mbalimbali ndani na nje ya nchi.

Aidha aliwapongeza TWCC katika kuunga mkono jitihada za Serikali kwa kuwawezesha na kuwainua Wanawake wafanyabiashara kote nchini.

"Ni wazi kuwa Mwanamke akiwezeshwa katika Biashara uchumi wake utaimarika na kumiliki kipato chake ataweza kuisaidia familia yake na kukuza uchumi wa familia na Taifa kwa ujumla" amesema Mhe. Kigahe.

Kwa Upande wake Mwenyekiti wa TWCC, Taifa Bi.Mercy Silla alisema kuwa Tuzo hizo ni sehemu ya maadhimisho ya siku ya Wanawake Duniani ambapo kila mwaka TWCC husherehekea kwa kuandaa maonesho ya Wajasiriamali.



# KITUO CHA UWEZESHAJI KAHAMA CHAENDELEZA MAFUNZO YA UJASIRIAMALI

KITUO cha Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi cha Kahama, Kahama Economic Empowerment Centre (KEEC) kimekuwa suluhisho la kupunguza changamoto za ajira kwa vijana kupitia mafunzo ya ujasiriamali kwa vitendo ambayo yanaendelea kutolewa bila gharama zozote katika kituo hicho.

Kituo hicho chenye jumla ya Taasisi 13, kimekuwa kikiendesha huduma za mafunzo kwa vitendo kupitia Shirika la kuhudumia viwanda vidogo (SIDO), Baraza la Taifa la Uwezeshaji Kiuchumi (NEEC), Chuo cha Ufundi stadi VETA, Chemba ya Biashara (TCCIA), Jukwaa la Wanawake, Chuo Kikuu Huria (OUT) na Kampuni ya Verd Mark Consulting Limited.

Miongoni mwa mafunzo yaliyotolewa katika kipindi cha kuanzia mwezi Januari 2023 mpaka Aprili, 2023 yanahusiana na Elimu ya Mifuko ya Uwezeshaji Kiuchumi, umuhimu wa kurasimisha biashara, utengenezaji wa sabuni, utengenezaji wa keki, utengenezaji wa mafuta ya kupaka, uchakataji wa vyakula na uandishi wa miradi.

Kituo pia kilifanikiwa kuwaunganisha wamiliki kumi wa viwanda katika Manispaa ya Kahama ili kushiriki Mafunzo ya Kaizen ambayo yaliendeshwa na SIDO Mkoa wa Shinyanga.

Akizungumza kuhusiana na program za mafunzo katika kituo cha Kahama, Katibu Mtendaji wa Baraza la Uwezeshaji, Bibi Beng'I Issa amesema kuwa huduma hizo za mafunzo zimekuwa zikitolewa kwa vijana ili kuwasaidia kuanzisha miradi yao mbambali ambapo wataweza kujisimamia na kutengeneza ajira kwa wengine.

"Tunahitaji vijana waweze kujisimamia wenyewe kwa kuanzisha miradi yao binafsi ambayo itawaongezea kipato wao na Serikali kwa ujumla lakini pia itatengeneza ajira kwa wengine"alisema Bibi Beng'i.

"Kituo cha Kahama kimekuwa kikiwapa mafunzo lakini pia mikopo yenye masharti nafuu ili waweze kupata mitaji na kuanzisha miradi"aliongeza.

Nae Afisa kutoka SIDO, Abel Beebwa ambaye amekuwa akiendesha mafunzo ya ujasiriamali kwa vitendo amewataka vijana hususani wa kanda ya ziwa kutumia fursa ya uwepo wao katika kituo ili waweze kuanzisha miradi yao binafsi na kujitegemea.

Wakati huo huo Meneja wa Mfuko wa Self Microfinance MF katika kituo cha Kahama, Bwana Edson Mwita amewataka vijana kuchangamkia fursa za mikopo inayotolewa na Taasisi hiyo ambayo ina masharti rafiki zaidi kwao.




# KITUO CHA KAHAMA CHACHOCHEA KASI YA KILIMO KANDA YA ZIWA TREKTA 26 ZATOLEWA KWA WAKULIMA

KITUO cha Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi cha Kahama (KEEC) ambacho kipo chini ya Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC) kimekuwa kimbilio la wakulima wa Kanda ya Ziwa kutokana na huduma zake.

Kituo hicho cha mfano Kitaifa ambacho kilianzishwa mwaka 2018 kina jumla ya Taasisi 13 za Uwezeshaji Kiuchumi ambapo pia zipo Taasisi mbili za Pass Trust na Mfuko wa Pembejeo wa AGTF ambazo zinahusika moja kwa moja katika kuwezesha wadau wa sekta ya kilimo kwa njia ya mikopo na ruzuku.

Taasisi zingine ambazo zipo katika kituo cha Kahama ni pamoja na Mfuko wa Self Microfinance Fund, Shirika la kuhudumia Viwanda la SIDO, Chuo cha ufundi stadi VETA, Benki ya NBC, Mamlaka ya kukusanya kodi (TRA), Chemba ya wafanyabiashara (TCCIA), GS1-Tanzania, Mfuko wa Pembejeo (AGITF), OSHA, Chuo Kikuu Huria (OUT), Kampuni ya Verd Mark, Jukwaa la Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi na Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC) ambayo ni Taasisi mama.

Taarifa rasmi kutoka Baraza la Taifa la Uwezeshaji zinaeleza kuwa katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2022/2023, kituo hicho kimefanikiwa kutoa jumla ya trekta 26 na Power Tiller 16 kwenda kwenye makundi mbalimbali ya wakulima wa Kanda ya Ziwa.

Katibu Mtendaji wa Baraza la Uwezeshaji, Bibi Beng'i Issa amesema kuwa nyenzo hizo zilizotolewa kwa wakulima zina thamani ya Shilingi Bilioni moja milioni mia nne hamsini na mbili (Tshs 1,452,000,000) zitaenda kuinua sekta ya kilimo kwa kukuza pato la wakulima na Serikali kwa ujumla.

Katibu Mtendaji huyo amesema kwamba Serikali ya Awamu ya Sita imedhamiria kwa dhati kupanua wigo wa ajira kwa Watanzania ambapo uwezeshaji huo uliofanyika utaleta matokeo chanya kwenye mnyororo wa thamani katika sekta ya kilimo na kuongeza tija.

"Serikali ina nia thabiti ya kuinua kipato cha wakulima na hizo nyenzo za kilimo zilizotolewa zitaleta matokeo chanya kwenye sekta ya kilimo na kupanua wigo wa ajira kwa Watanzania"alisema Bibi Beng'i Issa.

"Ni vema wazalishaji mali kutoka sekta zote wajenge tabia ya kutembelea vituo vya uwezeshaji kiuchumi ambapo huko watakutana na hizi fursa za mikopo yenye masharti nafuu na huduma zingine nyingi za kiuwezeshaji ikiwemo mafunzo na urasimishaji wa biashara"aliongeza.

Katibu Mtendaji alihitimisha kwa kuhimiza wanufaika wa mikopo kutoka katika mifuko ya Uwezeshaji kujenga tabia ya kufanya marejesho kwa wakati ili kusaidia wengine kupata fursa za kukopa.

# WATANZANIA 83,500 WANUFAIKA NA AJIRA MIRADI YA KIMKAKATI



TAARIFA rasmi kutoka Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC), zinaeleza kuwa jumla ya Watanzania 83,500 wamenufaika na fura za ajira katika miradi ya kimkakati inayotekelezwa hapa nchini.

Katibu Mtendaji wa Baraza hilo, Bibi Beng'i Issa amesema kuwa ajira hizo zimetokana na kazi zinazofanywa na NEEC ili kuongeza ushiriki wa Watanzania katika miradi ya kimkakati na uwekezaji.

"Tunashiriki katika majadiliano kuhakikisha katika kila mradi kunakuwa na mpango wa kuwashirikisha Watanzania," ameeleza Beng'i.

Pamoja na hilo, amesema kuwa kampuni 11,770 zinazomilikiwa na Watanzania zimeshirikishwa na kwamba malighafi za ujenzi zinazotumika kwenye miradi mbalimbali zinazalishwa na viwanda vilivyopo nchini.

"Takriban asilimia 70 ya nondo zinazotumika kwenye ujenzi wa reli ya kisasa (SGR) na nondo zinazotumika kwenye ujenzi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere (JNHPP) zinatoka Tanzania," ameeleza Beng'i.

Katibu Mtendaji huyo alihitimisha kwa kusema kwamba ushirikishwaji wa makampuni ya kitanzania umeongeza idadi ya viwanda vya vifaa vya ujenzi ambapo viwanda vya nondo vimeongezeka kutoka vitano hadi 10.

# NEEC YAFANIKISHA MRADI WA MAMA LISHE KAHAMA




*Mkuu wa Kituo cha Kahama, Jozaka Bukuku akitoa neno kwa Mama/ Baba Lishe*

BARAZA la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC), kwa kushirikiana na Manispaa ya Kahama na Jukwaa la Wanawake ngazi ya Wilaya limefanikiwa kuendeleza mradi wa Mama Lishe katika wilaya ya Kahama.

Mradi huo unalenga kuwapa Elimu Mama Lishe na kuwarasimisha ili waweze kutambuliwa na watoa huduma za kifedha ambapo wataweza kukopesheka lakini pia watafanya biashara zao katika mazingira yanayovutia zaidi.

Mradi huo unalenga kuufikia Mkoa mzima wa Shinyanga lakini hivi sasa umeanza na Mama Lishe 100 wa mfano katika Manispaa ya Kahama ambapo wameanza kupewa mafunzo kupitia kituo cha Uwezeshaji cha Kahama na wataalam wengine kutoka katika dawati la maendeleo ya Jamii.

Mama Lishe hao wamepatikana kupitia kanzidata ya Jukwaa la Wanawake ngazi ya Wilaya ambao walifanya zoezi la kuwatembelea na kuona changamoto wanazopitia kisha wakasajiliwa na kutambuliwa.

Akizungumza kuhusiana na mradi huo, Katibu Mtendaji wa Baraza la Uwezeshaji Bibi Beng'i issa amesema kwamba Mradi wa Mama Lishe unalenga kusaidia kundi hilo kutambuliwa na Taasisi za kifedha lakini pia kuwafanya wafanye kazi zao kwenye mazingira salama zaidi.
"Uwezeshaji haumuachi mtu yoyote nyuma na ndio maana hili kundi limeweza kufikiwa kwa lengo la kuinua huduma zao na kuwarasimisha waweze kutambuliwa na huduma za kifedha"alisema Bibi Beng'i.

"Tumeanza na kundi hilo la Mama Lishe 100 ambapo mbali na mafunzo wanayopewa lakini pia watasaidiwa kufungua makampuni ya usambazaji wa vyakula kisha kuwaunganisha na zabuni zinazopatikana katika Manispaa ya Kahama"alisema Katibu Mtendaji.

Mafunzo ya Mama Lishe hayo yamekuwa yakiendeshwa katika Kituo cha Uwezeshaji cha Kahama ambayo yalizinduliwa kwa mara ya kwanza na Mbunge wa Kahama, Mheshimiwa Kishimba.

# ZIARA YA NEEC KUHAMASISHA UTALII ZIWA TANGANYIKA





*Maafisa wa NEEC wakiwa katika ziara ya Utalii Ziwa Tanganyika Mkoa wa Kigoma*

ZOEZI la Maonesho ya sita ya Mifuko na Program za Uwezeshaji yaliyofanyika Mkoani Kigoma yalienda sambamba na ziara ya kitalii iliyofanyika Ziwa Tanganyika mwezi Mei mwaka huu.

Kamati tendaji ya Maonesho kutoka NEEC ilielekea usawa wa Ziwa Tanganyika kwa lengo la kujifunza historia nzima ya Ziwa hilo, shughuli zinazofanyika na matokeo ya Uwekezaji wa Mahotel uliofanyika kwenye fukwe za Ziwa kwa lengo la kujifunza.

Top Hill Hotel iliyopo kando ya Ziwa juu ya mlima ilikuwa moja kati ya sehemu zilizotembelewa na Kamati ya Maonesho.

Maeneo mengine ambayo yalitembelewa ili kuhamasisha shughuli za Utalii hapa Nchini ni pamoja na Hifadhi ya Gombe ambayo imekuwa maarufu kwa kuwa na idadi kubwa zaidi ya Nyani na Sokwe Mtu.

Hifadhi ya Gombe iliweka banda katika Maonesho na kutoa elimu kwa wanaotembelea ikiwa ni pamoja na kuwahamasisha umuhimu wa kutalii.

# MAHOJIANO MAALUM KWA KATIBU MTENDAJI

1 **Mwandishi**

Ni zipi kazi za msingi za Baraza la Taifa la Uwezeshaji Kiuchumi?

**Katibu Mtendaji**

Kazi mama ya Baraza la Uwezeshaji ni kusimamia na kuratibu Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ya mwaka 2004 ambayo inapaswa kutekelezwa na wadau wote wa Serikali kuanzia ngazi za Wilaya, Mikoa, ngazi za Kitaifa, wadau wa maendeleo na Sekta binafsi.

2 **Mwandishi**

Makao makuu ya Baraza yapo Dodoma, je mmewezaje kupanua huduma za Uwezeshaji ili kufikia namba kubwa ya Watanzania?

**Katibu Mtendaji**

"Ni kweli Makao makuu yapo Dodoma lakini tumeweza kupanua huduma za Uwezeshaji Kiuchumi kupitia madawati ya Uwezeshaji katika Halmashauri zote na Mikoa yote ya Tanzania Bara ambapo kuna waratibu wanaofanya kazi hiyo na walishajengewa uwezo".

Lakini pia kuna vituo 19 vya Uwezeshaji na lengo ni kila Halmashauri na Mikoa kuwa na vituo hivi ili kufikia idadi kubwa zaidi ya Watanzania".

3 **Mwandishi**

Kuna haya maonyesho ya Mifuko ya Uwezeshaji Kiuchumi mmekuwa mkifanya kila mwaka nini lengo lake hasa na yana tija gani kwa mtanzania mmoja mmoja na nchi kwa ujumla?

**Katibu Mtendaji**

Maonyesho haya yamelenga kuwasogezea wananchi karibu zaidi hizi huduma zinazotolewa na Mifuko ya Uwezeshaji KIuchumi na lengo hasa tunataka kupanua wigo wa fursa hizo ili ziweze kuwafikia watu wengi zaidi na kuwanufaisha.

Maonyesho yamekuwa yakifanyika Kikanda na muitikio umekuwa mkubwa katika kanda zote ambazo tumeshafanya katika Mikoa ya Dodoma, Mbeya, Morogoro, Simiyu, Arusha na mwaka huu yamefanyika Kigoma Mjini katika viwanja vya Mwanga.

4 **Mwandishi**

Kuna hii changamoto ya ajira kwa vijana na hasa wale wanaohitimu katika vyuo vyetu je Taasisi yako imechukua hatua zipi kukabiliana nalo mkiwa kama wasimamizi na waratibu wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Kiuchumi?

**Katibu Mtendaji**

"Kuna programu mbalimbali zilizoanzishwa kwaajili ya vijana na tumekuwa tukifanya program hizi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali yaani Serikali, wadau wa maendeleo na sekta binafsi".

"Baadhi ya program hizo ni pamoja na Kijana Jiajiri, Kijana Jiandalie Ajira, Program za Vijana wa JKT, 2jiajiri, Ajira yangu na Young Graduate Entrepreneurship Clinic.

Baraza pia limekuwa likitoa mbegu mtaji kwa washindi wanaowasilisha mawazo bora ya biashara ambapo program hii huwalenga zaidi wahitimu wa vyuo vikuu".

5 **Mwandishi**

Kuna miradi mbalimbali ya Kimkakati ikiwemo bomba la mafuta (East – Africa Crude Oil Pepeline-EACOP) ujenzi wa reli ya mwendokasi (Standard Gauge Railway (SGR) na mingine mingi, je mnawasaidia vipi vijana kunufaika na fursa zilizopo huko?

**Katibu Mtendaji**

"Kwa upande wa Bomba la mafuta ilianzishwa kanzidata maalum kupitia EWURA ambapo wamiliki wa makampuni madogo, ya kati na makubwa na yenye ujuzi katika maeneo mbalimbali yalihamasishwa kujisajiri ili yaweze kufikiriwa na kunufaika na zabuni na ajira zinazotolewa na Bomba hilo na matokeo yameanza kuonekana".

"Kupitia Mwongozo wa Ushiriki wa Watanzania katika miradi ya kimkakati yaani National Multisectoral Local Content Framework uliozinduliwa na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb) watanzania wengi hasa vijana wenye sifa stahiki wamenufaika kwa njia ya ajira katika miradi ya ujenzi wa Barabara, madaraja, Zahanati na hata migodini.

Vijana wamehamasishwa kujiunga katika vikundi vya uzalishaji mali yaani, "clusters" ili wawe na uwezo wa kutoa huduma katika miradi ya kimkakati na uwekezaji.

## 6 Mwandishi

Unalipi la kueleza vijana ambao ndio nguvu kazi ya Taifa?

**Katibu Mtendaji**

"Vijana wanapaswa kuwa wabunifu na wachapa kazi maana Taifa linawategemea hivyo pale ambao wanahisi mkwamo wasisite kuzisogelea fursa za Uwezeshaji zinazopatikana kuanzia kwenye ngazi za wilaya, Mikoa mpaka Taifa"

S.L.P 792, DODOMA
Simu: +255 22 2137362
Simu / Nukushi +255 22 2125596
Tovuti: www.uwezeshaji.go.tz
Barua pepe: neec@uwezeshaji.go.tz

uwezeshaji

uwezeshaji

uwezeshaji

uwezeshaji